# Title: Under the Mango Trees

**EPISODE 2**

**Author: Romie Singh**

**Editors: Susanne Fuchs, Katrin Ogunsade, Maja Braun**

## List of characters for episode 2:

- Narrator
- April
- Desirée
- Lorraine
- Endurance
- Teacher
- Children in background
- Students in background

## INTRO:

Karibu kwenye makala ya Noa Bongo jenga Maisha yako leo tumeingia katika sehemu ya pili ya mchezo wa redio kwa jina “Chini ya Miembe” mchezo huu unahusu mpango wa uzazi. Leo hii Desirée anamsaidia mdogo wake, Endurance, jinsi ya kukabiliana na matatizo ya shule lakini wakati huo huo anapokea habari nzuri kutoka kwa rafiki yake mpendwa f Lorraine kuhusu mashindano ya kutafuta kipaji katika TV yatakayo fanyika katika jiji la Granville.

**NARRATOR:** Desirée na Endurance walipanda basi kama kawaida yao kila siku asubuhi na mapema kuelekea shule ya upili ya Kentown High iliyoko kilometa 20kutoka kwenye kijiji chao cha Mtelera. Wanapofika shuleni, Endurance huwa amechoka sana kiasi kwamba hafurahii masomo yake . Mwalimu wake ameshalalamika mara nyingi kwamba kijana huyu hulala darasani na vilevile kuhusu harufu kama ya ngo’mbe inayokera sana . Hata hivyo, Desirée alipenda masomo na pia alipendelea sana kuimba na rafikiye mpendwa Lorraine, kila wakati wa mapumziko marafiki hawa walifanya mazoezi ya kuimba nyimbo wanazo zijua na mara nyingine walijaribu kutunga nyimbo mpya.

**<u>Sc.1 At school. Schoolyard ambience.</u>**

1. **SFX:** Background noise of boys and girls.

2. **SFX:** DESIRÉE /LORRAINE Practicing song (fade in)

3. DESIRÉE: (laughing) Hiyo ni nzuri sana!

4. LORRAINE: Itatubidi tumuimbie Bongo!

5. DESIRÉE: Bongo? Kwani yeye ni dufu dufu yaani mnene sana au amevaa ngozi ya mbuzi kichwani? (giggling)

6. LORRAINE: Hey! Des! Hilo ni jina la utani tu! Yeye ni mpiga ni mwanamuziki mzuri na pia mpiga drums hodari sana.

7. DESIRÉE: (apologetic) Whoops! Samahani sikujua kabisa!

8. LORRAINE: Ndio hivyo basi! Ni bora kuliko Yule rafiki wa kike, huyu jama ni kijana tena ni tajiri, hivi karibuni tu amefungua kampuni ya burudani katika mji wa Kentown sio mbali na hapa inaitwa Rainbow.But better than that girlfriend, he’s young and rich and has just opened up a new entertainment agency in Kentown. Just down the road from here, The Rainbow Agency.

9. DESIRÉE: Wow!

10. LORRAINE: Nakwambia! Basi yeye huandaa miziki na sauti za kila aima ya shughuli kama vile mashindano ya urembo, harusi na mambo mengi tu mimi nimesha jisajili kwake kama mwimbaji. Iwapo kutakuwa na bendi inayohitaji muimbaji basi Bongo ataniita ili kuona kama ninaweza kwa hivyo rafiki

| | | |
|---|---|---|
| | | yangu kama sisi tutaendelea vyema basi bila shaka tutaweza kuimba pamoja na ujue tutalipwa! |
| 11. | DESIRÉE: | Eti unasemaje? Yaani watu wanaweza kulipa kiingilio kwa kutaka kutusikiliza sisi tukiimba? (laughing) Loo sijui tutajiitaje? Au "The Hen Sisters!"? |
| 12. | LORRAINE: | Sawa! Basi! Kwa hivyo hutaki kujua kuhusu mashindano ya mkoa yaSo you don't want to know about the regional 'Pop Idols' competition ambayo Bongo anashiriki katika kuyatayarisha siyo? OK! Sawa tu! |
| 13. | DESIRÉE: | Uh? Sasa mwenzangu mimi sielewi Pop Idols ni nini? |
| 14. | LORRAINE: | Eti unauliza nini? Des! Please! Usiniambie eti kweli hujui kabisa nazungumzia kitu gani yaani huji Pop Idols wewe? |
| 15. | DESIRÉE: | Nafikiri wewe umesahau kuwa mimi naishi Mtelera – kule wenzio hatuna hata hiyo Televisheni , duh. Kwa tamko hilo nadhani hapo unajisikia vizuri sasa au siyo? |

16. LORRAINE: OK! OK! Samahani basi! Angalia nazungumzia kuhusu vijana wanapokutanika katika mchujo wa kutafuta mwenye kipaji kwa mfano kila mshiriki atahitajika kuimba mbele ya majaji watatu kwa hivyo ukipita raundi ya kwanza unachaguliwa kuendelea mbele na ikiwa hawakuridhika basi wana...

17. DESIRÉE: (makes clucking noises) ...wanatutupa nje na pengine watatuambia twende tukajaribu bahati yetu mahali pengine!

18. LORRAINE: (laughing) Des – Hebu wacha nikwambie! Zawadi rafiki yangu na mkataba wa kurekodi na fursa kibao za kurekodi matangazo na pia kufanya shoo za televisheni pamoja na kwenye steji yaani live kwenye jukwaa. Sisi ni wakali! Hebu sikilizaL! Jaribu kuja kwetu wiki endi hii mama yangu anakuulizia kila mara unajua alimpenda sana mama yako.  Kwa kweli angependa kukuona.

19. DESIRÉE: Lorraine - yaani umetia mkazo sana juu ya jambo hili! Hata na mimi ningependa sana kumuona tena Aunty Alice. Nina mambo mengi ninayotaka kumuuliza kumuhusu mama yangu.

20. LORRAINE: (softly) Lakini natumai hutagubikwa na majionzi Des, si ndio? Tunahitaji kuimba wew unajua tunahitaji kuimba nyimbo za furaha!

21. DESIRÉE: Nikipata majibu machache tu nadhani moyo wangu utaburudika sana, Lorraine. Ujue nyanya yangu ana matatizo yeye anakuwa mkali saa zote hasa kuhusu swala linalohusu jukumu la mwanamke nyumbani najua hatakubali mimi nitoke kwa sababu ya watoto nina hakika atanikataza lakini labda dada Bella atanisaidia!

22. LORRAINE: tafadhali hakikisha umepata ruhusa! Basi tuonane Jumamosi! Tutaimba na pia utapata fursa ya kukutana na Bongo! Nitampigia simu ili niweke miadi ya sisi kumuona halafu tutaendelea kutokea

hapo. Maisha yako yameanza upya SASA!

23. SFX: SCHOOL BELL

Kengele hiyo wacha niondoke! Tutaonana baadae!

**NARRATOR:** Desirée alikwenda darasi kwake pia lakini hakuweza tena kumakinika darasani. Mawazo yake yalimuwaza mama yake ambae alifariki mwezi mmoja tu uliopita. Kwa nini alikufa? Hilo lilikuwa ndilo swali alilotaka kumuuliza mama yake Lorraine ambae alifanya kazi katika kituo cha kupanga uzazi cha Kentown. Alikuwa daktari na alikuwapo wakati mama yake alipoaga dunia. Huku akiwa anaangalia nje kupitia dirisha la darasani, Desirée alikumbuka mazungumzo baina yake na mama yake wakati fulani ambapo Desirée kwa mara ya kwanza aliona nguo yake ya shule ina doa la damu.

24. **SFX:** MUSIC UP FADE AND HOLD UNDER SCENE

**<u>Sc. 2 Dreamlike</u>**

25. APRIL: Ah! Usifadhaike wala usiwe na wasiwasi Des! Damu hiyo ni ishara kuwa sasa umebadilika. Yaani umeanza kuwa na yai mwilini mwako.

26. DESIRÉE: (sounds younger) Eti nini? Nina mayai kama kuku?

27. APRIL: (laughing) Kitu kama hicho! Ila tu sisi wanawake tuna yai moja tu ambalo linakuwa mara moja kwa mwezi ndani ya kizazi. yaani ovaries tuna sehemu mbili za sehemu mbili ya kulia na kushoto hebu angalia!

28. **SFX:** Sound of paper

Unaona? Yai moja limejibanza hapa juu. Na kama yai hili halitapata rutuba basi linadondoka na kutoka nje na hiyo ndio damu utakayoiona kila mwezi– , Desirée. Kwa sasa mwili wako una uwezo wa kutengeneza yai na hiyo ina maanisha kuwa unaweza kupata mtoto isipokuwa najua huwezi lakini fahamu ya kuwa mwili wako unatoa nje lile yai ambalo halina rutuba kwa hivyo mwili ukifanya hivyo mwezi unaofuata yai jingine linakuwa katika upande ule mwingine na hali kama hiyo itajirudia kila mwezi hivyo basi matokeo yake ni kupata damu kila mwezi.

29. DESIRÉE: Yai linakuwa vipi mama!

30. APRIL: (gently) Rutuba.. yaani likipata rutuba...tuseme mwanaume..um oh.. hii itakuwa vigumu kidogo kueleza – hebu angalia picha hii. Nadhani umeshamuona nduguyo wa kiume akiwa hana nguo basi siku moja atakuwa na mke halafu si unaona hapa?

31. **SFX:** Sound of paper

Kwa hivyo baada ya kitendo hicho maji maji ya uzazi yataelekea moja kwa moja hadi kwenye lile yai lililo na rutuba ndani ya umbo la mwananamke na hapo maji maji hayo yatalirutubisha yai hilo kwa hivyo sasa yai halitadongoka kwa kuwa litakuwa limerutubishwa na matokeo yake ni mtoto. Na mara moja nikijua kuwa sikuona siku zangu za mwezi basi najua kuwa nimeshika mimba. Daktari Alice alishawahi kunieleza njia za kuzuia maji maji ya uzazi yasifike kwenye yai lakini njia hizi hazikukubalika hata kidogo.

32. MUSIC OUT

**<u>Sc. 3 In class</u>**

33. **SFX:** Class room ambiance

34. TEACHER: (off mic) Binti Thomas. Desirée! amka! Wala ulikuwa husikii kitu chochote nilikuwa nakwambia. Simama!

35. DESIRÉE: (off mic) Ndio mwalimu?

36. TEACHER: Hebu tafadhali gawa karatasi hizi za maswali moja kwa kila mwanafunzi.

37. **SFX:** Dissenting murmurs. Teacher claps hands for silence

Kimya. Nataka kila mmoja wenu aandike yafuatayo. Ni watu wangapi katika familia mnaishi pamoja nyumbani? Ni wangapi wanasoma? Shule yoyote ile yaani. Ni saa ngapi wanafunzi wanakwenda kulala? Je unafanya kazi zozote? Kama jibu ni ndio basi eleza unafanya kazi gani na kwa nini? Kwa ajili ya kupata fedha? Ujuzi? Au kwa ajili ya furaha tu? Soma maswali yote kwa makini halafu jibu.

38. DESIRÉE: halafu kutatokea nini mwalimuWhat will happen with it mwalimu?

39. **SFX:** (Class murmurs: What will happen. This is rubbish.What a stupid idea)

40. TEACHER: Shh. Mwalimu mkuu anataka walimu wote wafahamu hali halisi ya wanafunzi katika familia zao.

41. **SFX:** (Murmurs, groans)

Tunahitaji kuwasaidia wazazi na walezi wenu katika kufanikisha maendeleo mazuri ya wanafunzi wetu.

42. CLASS: (Laughter)

43. **SFX:** School bell

Tafadhali jazeni fomu hizo bila udanganyifu wowote halafu zirudisheni siku ya Jumatatu.

44. **SFX:** Scraping chairs. Children leaving class

45. TEACHER: (off mic) Oh, Desirée. Hebu njoo kidogo.

46. DESIRÉE: Naam mwalimu?

47. TEACHER: Endurance leo alikuwa na afadhali kubwa darasani hakutoa harufu ya kukera!

48. MUSIC UP

NARRATOR: Watoto wengi katika shule ya upili ya Kentown wanatoka mjini katika maeneo yaliyo karibu na shule . mara kwa mara walimkebehiEndurance'hasa kutokana na maisha yake ya kijijini na kufikia sasa hakutaka kuwapa fursa zaidi ya kuendelea kumchokoza. Desirée alipata wakati mgumu kumshawishi ajaze fomu waliyopewa shuleni walipokuwa ndani ya basi wakielekea nyumbani.

**<u>Sc. 4 Interior of bus</u>**

49. **SFX:** FADE IN VOICES AND SFX

50. DESIRÉE: Sikiliza, Bi Davies hawatawaeleza wamafunzi darasani kile tutakachokuwa tumejaza kwenye fomu zetu kwa hivyo hawatajua chochote.

51. ENDURANCE: Pengine watajua halafu watanicheka.

52. DESIRÉE: Angalia kama mtu yeyote akikucheka muulize anapata wapi maziwa, nyama na mayai yake?"

53. ENDURANCE: (grumpy) Si watasema kutoka sokoni tu.

54. DESIRÉE: (laughing) Basi huo ni ujinga nafikiri wanatania tu. Hata wewe una utani unaoweza kuwaenjoy kwa mafano je mkulima anhesabu ng'ombe zake vipi?

55. ENDURANCE (giggling): Mimi sijui mkulima anavyozihesabu ng'ombe zake?

56. DESIRÉE: (laughing) Si anahesabu na " cow-culator!"

57. **SFX:** groans and giggles

58. ENDURANCE: Oh, oh!

**NARRATOR:** Kichekesho kilisaidia! Lakini wakati walipofika nyumbani Endurance alikuwa amechoka sana hata hakuweza kuwatolea kichekesho chake watoto wanne wa mjomba wake

Blessing. Alilala hata kabla ya kujaza fomu yake na pia kufanya kazi zake nyumbani alizopewa shule. Nyanya alikuwa amechoka pia, basi Desirée aliwalaza watoto na baadae alitoka na kuelekea kwenye msitu wa miembe kama alivyofanya mara nyingi kwa ajili ya kuzungumza na mama yake.

**Sc. 5. Evening ambience**

59. **SFX:** Wind in the mango trees

60. DESIRÉE: Mama? Endurance anaendelea kulala darasani nyanya nae anafikiri labda eti anafanya kazi nyingo kwa hivyo anaona mimi nafaa kufanya kazi za shamba kwa hivyo niache shule.

61. APRIL: Endurance - mtoto wangu mdogo alikuja mapema mno ndio maana hana nguvu. Lakini usiache shule mwanangu. Tafuta njia unajua tunahitaji elimu.

62. DESIRÉE: Nafahamu mama. Ulikuwa ukisema kuwa hata wewe ulipenda sana kupata watoto wako baada ya kumaliza masomo yako. Bella anafikiria kurudia masomo, Mama! Anasema ilimbidi kuondoka kutoka

kwenye nyumba yetu yenye kelele nyingi. Sasa anaishi na Robert na anasoma kwa njia ya Posta pia anasema hataki watoto hivi sasa. Ma? Ma? Kwani umeondoka?

63. SFX: Winds in the trees

**NARRATOR:** taratibu, Desirée laliondoka kwenye msitu wa miembe huku mwezi ukipenyeza kwenye miti alijikuta anaimba nyimbo ambayo mama yake aliipenda sana, nyimbo ambayo aliitunga wakati ambapo yeyee, Bella na Endurance walipokuwa wadogo.

64. **SFX:** Des sings ‘signature tune’

**OUTRO.**

Hadi hapo ndio tumefika mwisho wa sehemu ya pili ya mchezo wa radio wa kusisimua kwa, jina “Chini ya Miembe” Umeandikwa na Romie Singh. Usikose kujiunga nasi katika sehemu ya tatu wakati ambapo Desirée hatimaye anapata nafasi ya kumuuliza daktari Alice vipi alivyokufa mama yake?.

Kumbuka kumueleza rafiki yako asikilize Noa Bongo Jenga maisha Yako. Ukitaka kuusikiliza tena mchezo huu fungua tovuti yetu anuani ni d w world dot d e mkwaju l b e.

Tukutane tena wakati ujao.

**END OF EPISODE TWO**